

SUALA LA UPOLE KATIKA FASIHI ANDISHI: UCHANGANUZI KATIKA RIWAYA YA PENDO LA KARAH (2014)

Agnes Mueni Muteti, Evans M. Mbuthia na Mary Ndung'u

Ikisiri

Makala hii inajadili suala la upole linavyojoitokeza katika riwaya ya Pendo la karaha iliyoandikwa na John Habwe (2014). Misingi ya riwaya hii imejielekeza katika ukiukaji wa ukawaida ulioko katika jamii. Vijana wanatamani nafasi za kazi ughaibuni. Wanapofika huko, wanakumbana na changamoto nyingi na matarajio yao hayafikiwi. Kudra, bintiye Riziki na mhusika mkuu, anakata tamaa kutokana na kauli anazopokezwa na wanaomzunguka; naye Kassim anakata tamaa kutokana na vitendo anavyotendewa na mamaye, Rehema. Nadharia inayoongoza mjadala huu ni nadharia ya upole iliyoasisiwa na Brown & Levinson (1987). Makala inabainisha kauli zenyе upole zinazotamkwa na wahusika mbalimbali, kuchunguza mikakati ya upole inayoteuliwa na wahusika katika mawasiliano yao na kutambua matendo yanayochangia kuwapo kwa upole katika mawasiliano baina ya wahusika. Kutokana na data zilizokusanywa, inaweza kuhitimishwa kuwa upole si suala la kiakademia tu, bali linaweza kuwa na umuhimu katika safu ya udiplomasia na katika masuala ya amani na maridhiano mionganoni mwa wanajamii katika mataifa yetu na hata kimataifa.

Utangulizi

Makala hii inajadili udhihirikaji wa upole kama unavyobainika katika riwaya kwa kutumia nadharia ya upole iliyoasisiwa na Brown & Levinson (1987) ili kupata maana kamili ya mawasiliano katika fasihi andishi. Makala inarejelea kauli mahususi za wahusika kama zinavyodhihirika katika riwaya ya *Pendo la karaha* (Habwe, 2014). Tunatumia misingi ya nadharia ya upole katika miktadha ya kimazungumzo ili kupata picha jumuishi ya suala la upole linavyoweza kujitokeza katika riwaya. Kutegemea miktadha mbalimbali, kauli za wahusika zinazodhihirisha upole zinaainishwa katika kategoria nne za upole zinazopendekezwa na Brown & Levinson (1987). Kategoria hizi zinawakilisha mikakati mahususi wa upole. Chini ya kila kategoria kuna njia mbalimbali zinazochangia kuwapo kwa kila mkakati. Kauli kutokana na *Pendo la karaha* zilichunguzwa ili kubaini mkakati wa upole unaobuliwa wakati wa mawasiliano kati ya wahusika.

Udurusu wa maandiko kuhusu mada

Lakoff (1973) alieleza kuwa kuna sheria mbili zinazoweza kuzingatiwa na wazungumzaji wanapowasiliana. Sheria ya kwanza ni ya uwazi ambapo msemaji anapaswa kusema mambo ya kweli yanayoweza kuthibitishwa moja kwa moja bila kupunguza wala kuzidisha. Sheria ya pili ni ya upole inayohusu msemaji kumpa msikilizaji uhuru wa kujiunga katika mazungumzo. Msikilizaji anapaswa kujihusisha na mazungumzo ya msemaji kwa hiari na wazungumzaji wanapaswa kuthaminiana katika mazungumzo. Katika makala, uwazi wa kauli za wahusika mbalimbali ulitusaidia katika kufahamu iwapo mhusika mahususi anadhihirisha upole au la.

Vilevile, Leech (1983) anaeleza upole kama tabia inayowawezesha wazungumzaji kuelewana na kudumisha mawasiliano katika muktadha maalumu. Leech (keshatajwa) anapendekeza kanuni sita muhimu za upole zinazoweza kufuatwa ili mazungumzo yaonekane kuwa yenyе upole. Kanuni ya mkakati inamhitaji msemaji kuzungumza kwa heshima na uangalifu. Mambo hayasemwi tu kwani kuna taratibu za kusema kwa udhibiti. Kanuni ya huruma inamhitaji msemaji kuzidisha huruma kwa msikilizaji; nayo kanuni ya kusifu inamhitaji msemaji kumpokeza msikilizaji kauli zenyе sifa na kujizuia kujisifu. Vivyo hivyo, kanuni ya kujitweza inamhusu msikilizaji kunyenyekua anaposifiwa. Kanuni kukubaliana inawahitaji wazungumzaji wakati wote kutafuta upenyu wa makubaliano iwapo wazungumzaji wanatofautiana katika usemi. Ni vyema kuwa na makubaliano kwanza kisha maelezo ya sababu ya kutofautiana. Isitoshe, kanuni ya ushirikiano inawahitaji wazungumzaji kushirikiana katika mazungumzo; na kanuni ya takrima inamhitaji msemaji kugharamika ili kumtoshelezea msikilizaji mahitaji yake. Kanuni hizi zinahusiana na mikakati ya upole inayoegemezwa katika makala kwa kuwa mikakati minne ya upole inategemea ujenzi wa uhusiano bora baina ya wazungumzaji kuititia kukubaliana, kusifiana, kujitweza, kuhurumiana na kushirikiana katika kuzungumza ili upole udhihirike.

Suala la upole vilevile limechunguzwa na watafiti mbalimbali ambao wamekita tasnifu zao kwenye tamthiliya, runinga na hata vipindi vyta redio. Raitania (2014) alifanya uchunguzi

kuhusu mikakati ya upole katika kipindi cha runinga. Uhusiano kati ya kazi ya Raitania (keshatajwa) na makala upo kwenye usawa wa kuchunguza upole wa wahusika katika mazungumzo kupitia misingi ya nadharia ya upole ya Brown & Levinson (keshatajwa). Machira (2015) alichunguza namna wahusika wakuu wanavyotumia mikakati ya upole katika tamthiliya. Utafiti wake unahusiana na mada ya makala kwa kuwa Machira (keshatajwa) amechunguza upole katika fasihi andishi anapoegemea tamthiliya na makala hii ilichunguza upole katika riwaya. Kadhalika, Ngisirei (2018) alichunguza umuhimu wa upole kwenye vipindi nya redio. Uchunguzi wake unaathiri mada ya makala kwa kuwa unatupa hamu ya kutafitia upole katika fasihi andishi kwa kuegemea riwaya. Gromov (2018) ni mionganoni mwa watafiti walitoa muhtasari wa kijumla kuhusu yanayojitokeza katika riwaya ya *Pendo la karaha*. Anaangalia riwaya za Habwe na kusema kuwa riwaya *Pendo la karaha* inahakiki jamii huku ikidhihirisha mwamko mpya wa wanajamii. Kazi hii tangulizi inaathiri mada ya makala hii kwa sababu suala la upole linaloweza kujitokeza mionganoni mwa wanajamii linaweza kuwekwa kwenye vitabu. Suala hili linaweza kudhihirika katika fasihi andishi kupitia kwa wahusika wanaoakisi wanajamii halisi.

Misingi ya kinadharia

Utafiti wa makala ina misingi yake katika nadharia ya upole iliy oasisiwa na Brown & Levinson (keshatajwa). Brown & Levinson (keshatajwa) wanafafanua upole kama hali ya kuyafanya mawasiliano yawezekane katika pande mbili zinazoweza kuzua ugomvi kwa kuepuka mvutano wa kimazungumzo. Wanaeleza kuwa upole unajumuisha msemaji anayeshiriki katika kuyaboresha mawasiliano na kuchukulia kuwa msikilizaji atafanya vivyo hivyo. Mihimili ya nadharia ya upole ni minne: kujali uso chanya, kujali uso hasi, kuwasilisha upole ndani ya rekodi na kuwasilisha upole nje ya rekodi.

Nadharia ya upole ilitanguliwa na nadharia ya uso iliy oasisiwa na Goffman (1967). Alieleza uso kama thamani ya kibinagsi inayojumuisha mwanajamii kujitokuza na kujipa sifa nzuri zinazokubalika katika utamaduni wa jamii yake. Uso unategemea hisia za wazungumzaji. Hisia zikiwa nzuri uso unaimarika na hisia zikikatizwa mwanajamii thamani yake inapungua.

Kupungua huku kunasababisha fedheha na uso kuharibika. Hisia za mwanajamii hutegemea mtazamo wa wengine kumhusu na mahusiano yake na wengine. Uso unapopotea humaanisha kuwa hisia za muonekano bora wa kijamii huwa zinaumbuliwa na uso unapopatikana, hisia za muonekano mzuri katika jamii huimarishwa.

Brown & Levinson (keshatajwa) waliipanua nadharia ya uso katika nadharia ya upole na kuigawa dhana ya uso katika sehemu mbili: uso hasi na uso chanya. Dhana ya uso chanya inamaanisha kuwa wakati wa mazungumzo, mzungumzaji hutaka kuonekana anafaa mbele ya wengine. Mshiriki katika mazungumzo anatamani kutambuliwa na mwenzake, kujumuishwa katika mambo na kusifiwa iwapo amefanya jambo nzuri. Dhana ya uso hasi nayo inarejelea kuwa mshiriki katika mazungumzo anadai uhuru wake. Wakati wa mawasiliano anapendelea kuwa huru kufanya uamuzi kuhusu mambo anayotaka. Aghalabu, mzungumzaji anatamani kuilinda faragha yake.

Brown & Levinson (keshatajwa) wanapendekeza mikakati minne ya upole itumike kukabiliana na matatizo ya mazungumzo ili nyuso za wazungumzaji ziimarike, kuhifadhika na hata kuboreka. Mikakati hii ni: mikakati chanya ya upole (MCU), mikakati hasi ya upole (MHU), mikakati ndani ya rekodi (MNdR) na mikakati nje ya rekodi (MNjR). Mikakati hii ikitiliwa maanani wakati wa mazungumzo, upole unadhihirika.

Uchanganuzi wa mikakati ya upole katika riwaya ya *Pendo la karaha*

Mikakati ya upole imetumika kwa njia anuwai katika riwaya ya *Pendo la karaha*.

Kuwapo kwa mikakati chanya ya upole (MCU)

Brown na Levinson (keshatajwa) wanaeleza kuwa mikakati chanya ya upole (MCU) inahusu msemaji kutambua mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji na kuyatimiza. Pia, msemaji anayashughulikia mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji ili kuendeleza mazungumzo. Baadhi ya mahitaji ni pamoja na msikilizaji kutambuliwa, kusifiwa, kupendwa na kushirikishwa katika mambo. Msikilizaji hapendelei kuaibishwa na kuudhiwa. Uhusiano kati ya wasemaji huwa wa kutendeana mazuri. Katika juhudzi za kudhihirisha MCU, msemaji hupunguza vitendo

vinavyoweza kuutisha uso wa msikilizaji na kumhakikishia kuwa anamthamini na kumhitaji. Msemaji anajichukulia kuwa katika kiwango sawa na msikilizaji na kumjumuisha katika mambo. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, njia sita zimedhihirisha kuwapo kwa MCU zikiwamo; njia ya kuwa na matumaini, kutambua mahitaji ya msikilizaji na kuyashughulikia, vitambulisho vya makundi, kutafuta makubaliano na kuepuka migogoro, kujumuisha wasemaji katika mambo na njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji.

Njia ya kutambua mahitaji ya msikilizaji na kuyashughulikia

Kipengele hiki kinahusu msemaji kutambua mahitaji ya msikilizaji na kutafuta namna ya kumtimizia mahitaji hayo. Katika mawasili, msemaji anatambua kitendo kinachowezza kumkasirisha msikilizaji na kukiepuka. Vile vile, msemaji anatambua athari ambazo zinaweza kutokea iwapo mahitaji fulani hayatashughulikiwa. Msemaji anaweza kumshirikisha msikilizaji kwa kumpongeza, kumsifu na kumdhahirisha kuwa anamjali. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, mahitaji ya Kudra yanashughulikiwa na Rehema, kama ifuatavyo:

“**Sawa, mwanangu. Niandikie jina lako hapa,**” Rehema alisema. “...**Kumbuka kuniachia nakala ya kitambulisho chako,**” Rehema alimweleza Kudra.
“**Nitafanya hivyo mama.**” Kudra alisema... (uk. 25).

Ni muhimu kutaja hapa kuwa Kudra ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Pendo la karaha*.

Yeye ni bintiye Riziki aliyekuwa mjane. Rehema anayeongea naye hapa ni wakala anayewasaidia wasichana kupata ajira ughaibuni. Kutokana na hali ya umaskini, Kudra alilazimika kumtembelea Rehema nyumbani kwake ili amsaidie kusafiri kwenda ughaibuni. Mazungumzo baina ya Kudra na Rehema yanadhihirisha kuwa Rehema anamjali Kudra. Wakala anaonekana kutambua mahitaji ya Kudra ya kupata ajira. Rehema anamsemesha Kudra kwa huruma na upole huku Kudra akifanya anavyoagizwa kufanya. Wote wanashirikiana katika kufanikisha usajili wa Kudra unaohitajika.

Njia ya vitambulisho vya makundi

Njia ya vitambulisho vya makundi inahusu msemaji kumuweka msikilizaji kwenye kategoria fulani kutegemea uhusiano wao. Makundi haya yanaweza kugawika katika misingi ya uhusiano

wa kiukoo, kirafiki, kinguvu au hata tofauti za kiumri, ili kudhihirisha heshima. Katika kutumia njia hii, msemaji anaonesha uhusiano uliopo kati yake na msikilizaji kwa kutaja kikundi anachomjumuisha. Baadhi ya maneno yanayoweza kutumiwa kama vitambulisho makundi ni; dada yangu, mwanangu, mama yangu, mionganini mwa mengine. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, vitambulisho vya makundi vinadhihirika katika mazungumzo kati ya Rehema na Kudra ili kuwasilisha MCU kama ifuatavyo:

“Karibu mwanangu.” Kudra alikaribishwa na Rehema. **“Ahsante, bibi.”** Kudra alisema. **“Nikusaidie vipi mwanangu?”** Rehema alimuuliza Kudra. **“...Ni kweli mwanangu...”** Rehema alishauri akitabasamu. **“N’kutilie chai mwanangu?”** Rehema alimuuliza Kudra. **“Usijisumbue, mama.”** Kudra alijibu. **“Keziah?”** **“Mletee mgeni angalau maji ya limau. Mwanangu usikatae kula au kunywa. Mimi ni mamako”** (uk. 22-24).

Kutokana na mfano huu, ni bayana ya kwamba Rehema anafanya juhudini za kuhakikisha kuna uwiano baina yake na Kudra na kumrejelea kama mwanawe. Rehema anamrai Kudra ili anywe chai na kula bila woga kwani yeye ni kama mama yake. Japo kuwa Riziki ndiye mama yake halisi Kudra, Rehema anajipa nafasi hiyo ili kuleta uhusiano mzuri baina yao. Kudra naye anamtambulisha Rehema kama mama, jina la adabu anapomueleza Rehema kuwa hahitaji kinywaji chochote. Kwa ujumla, dondo linaonesha wazi namna wazungumzaji hawa wanavyoshirikina na kutamkiana kauli zenye upole.

Njia ya kutafuta makubaliano na kuepuka mgogoro

Kulingana na Brown na Levinson (keshatajwa), makubaliano katika mazungumzo hupatikana kupitia kwa kuwasilisha mambo yanayokubalika kwa wazungumzaji. Msemaji hutambua mambo yanayoweza kuridhiwa na msikilizaji na kuyatekeleza. Mambo hayo yanapotekelezwa, uhusiano kati ya wazungumzaji huimarika. Makubaliano yanatokea ikiwa mahitaji ya msemaji katika mazungumzo ni sawa na yale ya msikilizaji. Mchakato mzima wa makubaliano unapotokea, MCU hudhihirika. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, njia ya kutafuta makubaliano na kuepuka mgogoro inajitezea katika mazungumzo kati ya Kudra na Riziki kama ifuatavyo:

“Sidhani hivyo mama. Si kwa ubaya. Mimi ninataka kazi kwanza...” Kudra alimueleza mama yake msimamo wake. **“Utakavyo mwanangu. Mungu akujaaliye fungu la Baraka. Akufikishe utakako. Akupe hitaji la moyo wako.**

Mimi kama mamako nakupa radhi zangu mimi na za marehemu baba yako, Mzee Sanga.” Riziki alisema (uk. 29).

Ni bayana kwamba katika mfano huu Kudra na Riziki wanajaribu wawezavyo kuteua maneno yatakayohakikisha maridhiano kati yao yanapatikana. Ni katika hali ambapo wote wana msimamo tofauti kuhusu ndoa. Riziki anampendekezea binti yake kuolewa ila Kudra anaona ni bora kutafuta pesa kabla ya kuolewa. Kudra anaeleza kutofautiana kimawazo na Riziki anaposema, “**Sidhani hivyo mama. Si kwa ubaya. Mimi ninataka kazi kwanza...**” Riziki anatambua uwezekano wa mgogoro na kuuepuka anaposema, “**Utakavyo mwanangu...**” yaani utakavyoamua hata kama hukubali rai yangu. Kutokana na alivyoianza kauli, Riziki aliweka wazi kuwa alimpa Kudra uhuru wa kufanya alichoridhia bila pingamizi yoyote na kumpa baraka zake na za marehemu Mzee Sanga, baba yake Kudra.

Njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji

Njia hii inahusu msemaji kuchagua na kushiriki katika mada inayomvutia msikilizaji ili kudumisha uso chanya wa msikilizaji. Mada ya aina hii inapochaguliwa, uwezekano wa msemaji kumuudhi msikilizaji haupo kwa sababu yanayozungumzwa yanaendana na mahitaji ya msikilizaji. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, njia ya kuteua na kuchangia mada inayomvutia msikilizaji inadhihirika katika mazungumzo kati ya Kidawa na Riziki, kama ifuatavyo:

“Dadangu habari za Kudra?” Kidawa alimuuliza. **“Kudra hatumsikii. Hupiga mara chache. Mkubwa wake hataki awasiliane na watu nyumbani sasa,”** Riziki alisema akiwa amejishika tama (uk. 122).

Dondoo hili linahusu mjadala wa marafiki. Kidawa ni rafiki na jirani yake Riziki. Baada ya Kudra kuondoka kwenda ughaibuni, alihakikisha kuwa anajitahidi kumjulia hali Riziki mara kwa mara na kumuuguza alipokuwa mgonjwa. Katika mfano huu, Kidawa anaiteua mada inayoiteka makini ya Riziki huku akimpa nafasi ya kujieleza. Riziki alipendelea mada kumhusu binti yake ili kuupunguza upweke aliokuwa nao. Kidawa anapoiteua mada kumhusu Kudra, Riziki anaichangia vilivyo. Ni wazi kuwa uteuzi wa mada alioufanya Kidawa unaibua ushirikiano katika mazungumzo yao na urafiki wao unadumu.

Njia ya kujumuisha msemaji katika mambo

Kulingana na Brown & Levinson (keshatajwa), makini ya msikilizaji inatekwa pale tu anapojumuishwa katika mambo na msemaji. Mambo ambayo msemaji anajumuishwa kwayo ni mambo anayoyafurahia au anayoonesha kupendezwa nayo. Muktadha wa mazungumzo huwa umeeleweka vizuri baina ya wazungumzaji ili MCU udhirike wazi. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, kiambishi tu- cha wingi kinadhihirika katika kauli za Riziki na Subira wanapojumuishana katika mambo kama ifuatavyo:

“Siri dadangu wajua. Ni yule mwanangu Rukia. Tangu apate hicho kikazi chake Dubai, ametuweka vizuri... **Tunamshukuru Maulana.**” Subira alisema “... Rukia ni mtoto mwema..., atachuma tende **atuletee nyumbani.**” Riziki alisema. “**Tunamuombea kila la heri**” (uk. 14-15).

Subira ni mama yake Rukia, msichana aliyemtangulia Kudra kwenda ughaibuni. Maisha ya Subira yalikuwa yameboreka baada ya binti yake kupata kazi ughaibuni. Kutokana na mfano huu, Subira anasema, “...ametuweka vizuri.” Subira anamueleza Riziki mambo yalivyo nyumbani kwake na kumjumuisha kama mmoja katika familia yake anaposema, “**Tunamshukuru Maulana.**” Riziki alitaka kujinasibisha na ufanisi huu. Alijijumuisha kwa kumpa Rukia sifa tele huku akisema, “...Rukia ni mtoto mwema mwenye nemsi, atachuma tende **atuletee nyumbani.**” Riziki alitumia kiambishi *tu-* katika kujijumuisha kama mmoja wa familia ya Subira anaposema, “**Tunamwombea kila la heri, dadangu.**” Riziki alijishirikisha kwa kumtakia Rukia mazuri. Katika kauli zao, wanadhihirisha kuthaminiana kama dada ilhali hawana uhusiano wowote wa kiukoo. Ushirikiano baina yao unachangia kufanikisha mawasiliano na MCU wa upole unadhihirika wazi.

Njia ya kuwa na matumaini

Njia ya kuwa na matumaini inahusu msemaji kuwa na matarajio wakati wa mazungumzo. Njia hii inachangia msemaji kuuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kumpa tumaini kuwa anaweza kupata anachotamani. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, njia ya kuwa na matumaini mema inachangia kudhihirisha MCU katika mazungumzo kati ya Kudra na Rehema kama ifuatavyo:

“Nina kazi nzuri mwanangu. Utaifanya miaka miwili tu kisha utatajirika. Utaweza hata kuwasaidia jamaa zako.” Rehema alisema. **“Naomba iwe hivyo mama. Mzee wangu hawezi kujimudu. Ananitegemea mimi kwa kila kitu; chakula, dawa na kodi ya nyumba.”** Kudra alisema (uk. 63).

Mfano huu unadhihirisha kuwa kauli inayotamkwa na Kudra inampa matumaini kwani alitamani kupata kazi ughaibuni. Kudra anatamani kuwa na pesa nyingi kama wasichana wengine walioenda Dubai kufanya kazi. Rehema anapomueleza Kudra kuwa ana kazi nzuri, Kudra anapata mwanga wa matumaini. Rehema anazidi kueleza **“...Utaifanya miaka miwili tu kisha utatajirika...”**. Kudra alitamani kutajirika ili aibadilishe hali yake ya umaskini katika familia yake. Kudra anatazamia kupata kazi nzuri huku akisema **“Naomba iwe hivyo mama. Mzee wangu hawezi kujimudu. Ananitegemea mimi kwa kila kitu; chakula, dawa na kodi ya nyumba.”** Kudra anadhihirisha furaha na matumaini yake. Matumaini ya Kudra kujisajili upya yanajengeka kupitia kauli anazopokezana na Rehema.

Kuwepo kwa mikakati hasi ya upole (MHU)

Kulingana na Brown & Levinson (keshatajwa), mikakati hasi wa upole (MHU) inajumuisha msemaji kuyatambua mahitaji ya uso hasi wa msikilizaji na kuyatimiza. Msemaji anayapunguza mahitaji na matamario yake kutoka kwa wengine. Msemaji hufanya hivyo kwa kumpa msikilizaji uhuru na nafasi ya kujieleza. Mahitaji ya uso hasi wa msikilizaji yanajumuisha kutotaka kujihusisha na wengine, kushirikishwa katika mambo na kutotaka kupokea msaada wowote kutoka kwa msemaji. Msikilizaji anapotendewa mambo haya anahisi kuwa anasumbuliwa. Msikilizaji hapendelei kushirikishwa katika kuulizwa maswali, kupewa ushauri, kuombwa au hata kuelezwu mambo. Msikilizaji anataka nafasi yake iheshimiwe na asijumuishwe kwa lolote bila yeye kuridhia. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, MHU umejidhihirisha kupitia njia zifuatazo: kuomba msamaha, kutaja mambo kwa ujumla, kudhihirisha heshima baina ya wazungumzaji, kukosa matazamio na kutoa ubashiri wa matokeo mabaya.

Njia ya kuomba msamaha

Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, njia ya kuomba msamaha inadhihirika katika mazungumzo baina ya Kudra na Nayrat kama ifuatavyo:

“Nilikuwa namwamkua tu yule jirani.” Kudra alisema. “Ulikuja kufanya kazi ama kuamkuana?” Nayrat aliuliza. **“Pole, sitarudia tena,”** Kudra aliomba radhi. “Singependa urudie kosa hilo tena.” Nayrat alimweleza (uk. 94).

Katika nukuu hii, Nayrat ni mwajiri wa kwanza wa Kudra. Kutokana na mfano huu, Kudra alikuwa amenyimwa uhuru na mwajiri wake wa kuzungumza na majirani bila ruhusa. Nayrat alighadhibika baada ya kutambua kuwa Kudra alizungumza na jirani, kinyume na amri yake. Kudra alitambua kuwa alimkosea Nayrat na kuwa na uso hasi. Kudra alimwombwa Nayrat msamaha bila kusita kwa kusema, **“Pole, sitarudia tena.”** Ombi hili linaupunguza uwezekano wa makabiliano mengine kuzuka kwani ghadhabu ya Nayrat ilipungua. Hatimaye, Nayrat anamkumbusha Kudra agano lao la kutoongea na majirani bila kupewa ruhusu na mwajiri.

Njia ya kutaja mambo kwa ujumla

Brown & Levinson (keshatajwa) wanaeleza kuwa kutaja kauli kwa ujumla ni kusema kwa kujumuisha ili kuwasilisha kikundi mahususi cha watu. Kauli za msemaji hazinuiwi kumlenga mtu ye yote mahususi moja kwa moja. Kwa kutumia ujumla, msikilizaji anaupokea ujumbe bila kutiwa aibu au kuvunjiwa heshima mbele ya watu. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, njia hii inadhihirika katika mazungumzo kati ya Rehema na Kassim kama ifuatavyo:

“Nisikilize tu, sikukatizi kunywa wala kufanya lolote la utashi wako. Lakini rudi nyumbani.” Rehema alimrai Kassim... (uk. 80).

Katika nukuu hii, tunaona Rehema akiongea na mwanawe, Kassim. Alikuwa ametoroka nyumbani na kuanza kujihuisha na matumizi ya madawa ya kulevyta. Kutokana na mfano huu, Rehema anataja kwa ujumla mambo ambayo Kassim anajishughulisha nayo ili kumtuliza Kassim aliye potoka asije akafikiria kuwa anasutwa au kudhihakiwa. Kwa upande mwingine, Kassim alifahamu upungufu wa Rehema ila aliamua kusema kwa ujumla kuwa hakutaka kurudi nyumbani. Badala ya kumrejelea Rehema moja kwa moja kuwa atahukumiwa kwa vitendo vyake, Kassim aliitafuta njia mwafaka ya kuufikisha ujumbe wake bila kumsababishia mama yake fedheha.

Njia ya kudhihirisha heshima baina ya wazungumzaji

Kwa mujibu wa Brown & Levinson (keshatajwa), njia ya kudhihirisha heshima inajumuisha msemaji kuiweka thamani ya msikilizaji mbele wakati wa mazungumzo. Thamani hii inawekwa kwenye misingi ya tofauti za kiumri, uhusiano, cheo, nguvu na mamlaka. Ulazimishaji unachukua nafasi ya heshima katika muktadha wa mawasiliano na uso hasi wa wazungumzaji unahifadhiwa. Naye, Yule (1996) anaeleza kuwa msemaji mwenye hadhi ya chini hudhihirisha tofauti kubwa kati yake na msikilizaji mwenye hadhi ya juu. Uhusiano wa wazungumzaji unachangia sana wanachokisema kwa hivyo sifa za uhusiano wa kuwa karibu kati ya wazungumzaji kwenye misingi ya umri na nguvu ni muhimu kuchunguzwa. Msemaji anaweza kutumia majina ya heshima ili kuepuka uwezekano wa ugomvi kuibuka na kukithiri. Kwa mfano, katika riwaya ya *Pendo la karaha* (uk. 146), maneno ya Salim yanaafiki heshima kati yake kama mwajiri na Kudra, mwajiriwa. Bw. Salim ni mwajiri wa pili wa Kudra. Salim alimpa Kudra maelezo kwa utaratibu kuwa alikuwa amemuachisha kazi baada ya mgogoro uliozuka baina ya Hanawi, binti yake na Kudra. Japo kuwa Kudra hakuridhia uamuzi wa mwajiri wake, aliyaheshimu mahitaji ya uso hasi wa Salim na kuondoka kama alivyoamrishwa bila kuzua zogo.

Kukosa matazamio

Kulingana na Brown & Levinson (keshatajwa), njia ya kukosa matazamio inajumuisha msemaji kupoteza matumaini ya kupata vitu au mambo ayatakayo. Msikilizaji akikosa matazamio atauhifadhi uso hasi wake kwa sababu hatatarajia kupotezwa mambo na msemaji. Iwapo patatokea jambo, msikilizaji hataathirika kwa vyovyote vile kwa sababu hatilii makini kile anachokisema msemaji. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, njia ya kukosa matazamio inajitokeza kudhihirisha MHU katika mazungumzo kati ya Rehema na Kudra kama ifuatavyo:

“Hutaki kwenda mwanangu? Nimekuchukulia hadi viza mwanangu.”
Rehema alimwambia Kudra... “**Sitaki.**” “**Kisa mwanangu? Nina mwajiri tayari. Nauli ya ndege ishalipwa...**” Rehema alisema. “**Sitaki kwa sasa mama. Samahani**” (uk. 55-56).

Kutokana na mfano huu, Rehema alimrai Kudra akubali kusafiri ila Kudra alidhihirisha wazi kuwa hakutamani tena kusafiri. Kudra anatamka, “**Sitaki kwa sasa mama. Samahani.**” Japo kuwa maneno ya Kudra ni kinyume na alivyotarajia Rehema, anayatamka kwa uangalifu.

Kudra anajumuisha radhi katika kauli yake hasi. Jibu la Kudra linadhihirisha upole na hali yake ya kupoteza hamu ya kushirikishwa zaidi katika safari ile. Katika kuafiki maneno yake, Kudra anaondoka haraka nyumbani kwa Rehema.

Kuwapo kwa mikakati ndani ya rekodi (MNdR)

Kulingana na Brown & Levinson (keshatajwa), mikakati ndani ya rekodi (MNdR) hujitokeza baina ya wahusika wenyewe mahusiano ya karibu na waliozoeana kwa kiasi fulani. Kauli za moja kwa moja hutolewa na wazungumzaji waziwazi bila kuficha chochote. Wazungumzaji wanaweza kutaniana ila sharti msemaji amakinike kuuhifadhi uso wa msikilizaji. Wakati mwingine, mahitaji ya uso huwekwa kando ili kushughulikia tukio la dharura linalozuka. Mahitaji ya uso yakiwekwa kando msikilizaji huweza kunufaika kuitia ahadi zinazotolewa na msemaji na heshima wanayodhihirishiana. Lengo kuu katika MNdR ni kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na kuzua ushirikiano wakati wa kuitisha ujumbe muhimu.

Njia ya kushughulikia dharura

Kushughulikia dharura kunatokea iwapo katika mazungumzo jambo linalotokea halikuwa limetazamiwa. Wazungumzaji wanayaweka mahitaji yao kando ili kulishughulikia jambo hilo. Msemaji anaweza kutekeleza MNdR kwa kumuonya msikilizaji dhidi ya kitu kinachoweza kumsababishia uchungu au mateso. Njia hii inadhihirika katika riwaya ya *Pendo la karaha* (uk. 81-82) kuitia kauli za Rehema kwa mumewe, Mzee Choka. Rehema alikuwa katika hali ya upweke baada ya kumfukuza mumewe na Kassim, mwanawe wa kipekee kutoweka na kuanza kutumia mihadarati. Dharura iliyohitajika kushughulikiwa ni upweke wa Rehema, maradhi yake ya moyo na hali duni ya Kassim. Baada ya Rehema kumpata Mzee Choka, aliyateua maneno mwafaka na kumhakikishia kuwa alimhitaji. Hali ya Kassim ilihitaji juhudzi za wazazi wote ili kupata mwelekeo bora wa maisha. Wote walishirikiana kumrai Kassim kurudi nyumbani na kuyajenga maisha upya.

Njia ya kukabiliana na tofauti za kimamlaka

Kulingana na Brown & Levinson (keshatajwa), tofauti za kimamlaka kati ya msemaji na mpokezi wa ujumbe zinajitokeza kupitia kwa maneno yanayotamkwa na watusika mbalimbali. Katika kudhihirisha MNdR, aliye chini kimamlaka mara nyingi hudhihirisha heshima kwa anayemzidi cheo au nguvu. Njia hii inadhihirika katika riwaya ya *Pendo la karaha* (uk. 92- 93) kupitia kauli za Kudra kwa mwajiri wake wa kwanza. Bw. Aminii ana nguvu za kimamlaka dhidi ya Kudra kwa hivyo, Kudra hana budi kumheshimu. Baada ya Kudra kupokea habari kuhusu maradhi ya mama yake; Riziki, aliwaeleza waajiri wake kuwa aliwahitaji wampe fedha za kumwezesha kumuuguza Riziki. Kudra anatamka kauli zake kwa uangalifu na heshima kubwa kwa Aminii. Unyenyekevu wa Kudra unamwezesha Aminii kumjuza kuwa wangelifikiria ombi lake. Mazungumzo kati yao ni wazi na maafikiano yanapatikana katika pande zote mbili.

Muktadha wa kumnufaisha msikilizaji

Kumnufaisha msikilizaji katika mazungumzo kunahusisha msemaji kutoa usemi kwa lengo la kumfaidi mpokezi wa ujumbe kwa kumdhiihirishia wazi ukarimu. Msemaji anaweza kujitolea kumsaidia msikilizaji na kumuonesha ukarimu kama alivyoeleza Leech (keshatajwa) katika kanuni ya takrima. Isitoshe, maneno yanayosemwa yanahitaji kuwasilishwa kwa idadi tosha na kwa namna inayoepuka utata kama alivyopendekeza Grice (1975). Katika riwaya ya *Pendo la Karaha*, kunufaika kwa msikilizaji kunadhihirika katika mazungumzo kati ya Riziki na Kidawa kama ifuatavyo:

“Pole Dadangu.” Riziki alimueleza Kidawa aliyejewa taabani... (uk. 30).

Kutokana na mfano huu, mazungumzo haya yanatokea baada ya kifo cha Lindo, mwanawe Kidawa. Japokuwa Kidawa alikuwa amempoteza Lindo, alijikaza. Riziki alimtamkia Kidawa kauli hii: **“Pole Dadangu”** na kumnufaisha kupitia kumfariji na majonzi ya Kidawa yakapungua. Kwa kauli hii ya upole ni wazi kuwa mwandishi anaonesha wazi Riziki anamdhiihirishia Kidawa kuwa anamjali.

Muktadha wa kutoa ahadi kwa msikilizaji

Kulingana na Brown & Levinson (keshatajwa), kutoa ahadi kunahusisha sharti ambalo msemaji hujipa ili kulitimiza kwa msikilizaji. Katika mazungumzo, anayeahidi anakabiliwa na jukumu la kutekeleza agano kwa manufaa ya anayeahidiwa. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, wakala Rehema anampa Rukia, binti yake Subira ahadi ya kuipata kazi kama ifuatavyo:

“Njoo mwanangu nikupe kazi.” Alisema Rehema... **“Kazi gani mama?”** Rukia alimuuliza Rehema. **“Kazi ya Uarabuni, Bi. Mdogo. Kazi hasa wala sio huu utumwa wa Rajiv usiokufaidi.”** (uk. 5).

Kutokana na mfano huu, Rehema anaahidi kumpa Rukia kazi. Rehema alitumia maneno ya kuvutia ili kumrai Rukia aliposema **“Njoo mwanangu nikupe kazi.”** Rehema alisisitiza uzuri wa kazi aliyompendekezea Rukia kwa kusema **“Kazi ya Uarabuni, Bi. Mdogo. Kazi hasa wala sio huu utumwa wa Rajiv usiokufaidi.”** Rehema alifahamu kuwa Rukia alikuwa na mahitaji mengi ila kazi aliyoifanya haingemwezesha kujikimu. Rehema aliamua kumpa Rukia nafasi ya kazi ughaibuni ili aweze kuyabadilisha maisha ya umasikini.

Kuwepo kwa mikakati nje ya rekodi (MNjR)

Brown & Levinson (keshatajwa) wanaeleza kuwa mikakati nje ya rekodi (MNjR) inahu su uhuru wa wazungumzaji katika mawasiliano. Maneno ya msemaji hayamfungi kwa kile anachokisema kwa sababu anasema kwa mzunguko na kufumba; bila uwazi. Msemaji hawezu kuchukuliwa kuwa aliahidi kufanya jambo fulani kwa sababu hakuna ushahidi. Mahitaji ya msemaji yanatajwa tu na msikilizaji huhitajika kufasiri kinacho semwa. Msikilizaji kwa uelewa wake anahisi kuwa ana jukumu la kumtimizia msemaji jambo fulani. Maana ya kauli ya msemaji kwa kiwango fulani inaweza kujadiliwa kwa sababu mawazo ya msikilizaji yanatanda katika uelewa wa kile anachodhani msemaji anakimaanisha. Ufasiri wa ujumbe anaousikia msikilizaji unategemea uelewa wake. Msikilizaji anaweza kuufasiri ujumbe tofauti na namna msemaji anavyomaanisha na kwa kiasi fulani kuuepusha ugomvi katika mazungumzo. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, MNjR inadhihirika katika kutumia maswali ya balagha, mdokezo na kinaya kwa lengo la kuzua utata.

Njia ya kutumia maswali ya balagha ili kuzua utata

Maswali ya balagha ni aina ya maswali yanayodhihirika katika mazungumzo ila hayahitaji majibu kutoka kwa wazungumzaji. Maswali haya yanapojitokeza yanajenga mawazo ya msikilizaji na fasili ya anachokimaanisha msemaji anaposisitiza jambo. Maswali haya yanazua utata unaomfanya msikilizaji kuyaona mambo kupitia muona ulimwengu wa msemaji. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, maswali ya balagha yanaendeleza MNjR katika mazungumzo kati ya Rehema na Kassim, kama ifuatavyo:

“Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi? Mama yangu yuko Ujerumani.”

Kassim alisema. “...Nisamehe Mwwaaaa...” Rehema pumzi zilimwisha.

“**Nikusamehe nini?**” (uk. 80).

Mfano huu unaibua utata wa hali ilivyo katika uhusiano wa Rehema na Kassim. Maswali yanayotumiwa na Kassim yanamfikirisha Rehema bila kumkosea heshima. Kassim anamuuliza Rehema **“Kama ni mamangu? Tena mamangu yupi?...”** Kassim anampitishia Rehema ujumbe kuwa amezembea kutekeleza wajibu wake kama mama na kumtaka Rehema abadili mienendo yake. Kassim anapoombwa msamaha na Rehema, alimuuliza **“Nikusamehe nini?”** Kassim aliweka wazi kwamba iwapo Rehema angebadilisha tabia yake ya ulaghai, angemsamehe. Kupitia kwa maswali haya, Rehema anafasiri kuwa alihitaji kuubadili mwenendo wake.

Njia ya kudokeza mambo ili kuzua utata

Kulingana na Senkoro (2011), mdokezo ni njia ya msemaji kukata maneno katika mazungumzo badala ya kutamka kauli kamili zinazoonekana wazi na kwamba msikilizaji ana uwezo wa kung’amua yaliyokusudiwa na msemaji. Msemaji anadokeza jambo hatua kwa hatua bila kulisema bayana. Kusema huku kunajenga utata. Mbinu ya kudokeza inahusu msemaji kumtayarisha msikilizaji kuupokea ujumbe unaoweza kuudhuru uso wake. Njia ya mdokezo inafanikishwa katika riwaya ya *Pendo la karaha* (uk. 148) kupitia kauli za mdokezo za Dele na Kele, waajiriwa wa miaka mingi nyumbani kwa Bw. Salim. Wanamdokezea Kudra ili kuacha mahusiano ya kimapenzi na Salim, mwajiri wao ila Kudra alidhani kuwa walimfanyia mzaha.

Baada ya kuachishwa kazi, Kudra anatambua maana halisi ya vidokezo katika kauli za Dele na Kele.

Matumizi ya kinaya ili kuzua utata

Wamitila (2008) anaeleza kinaya kama njia ya msemaji kutumia maneno ili kuzua maana inayopingana na yale anayonuia kuyawasilisha kwa msikilizaji. Aghalabu, msemaji husema kinyume na anavyotarajia msikilizaji ili kudhihirisha kinaya. Msikilizaji huwa na jukumu la kushirikiana na msemaji ili kutambua kinyume cha kile anachokimaanisha msemaji. Ushirikiano kati ya wazungumzaji ni muhimu ili kutambua kinachosemwa. Katika riwaya ya *Pendo la karaha*, MNjR unadhihirika kupitia kauli ya Kidawa kwa Lindo kama ifuatavyo:

“Kama unataka kulewa, lewa kabisa hiyo dawa ya unga ikuue, tutakuzika maana huna faida.” Kidawa alimueleza Lindo (uk. 11).

Katika nukuu hii tunaona kuwa Lindo, mwanawe Kidawa alikuwa amezama katika matumizi ya madawa ya kulevya. Kutohana na mfano huu, hatua zilizofuata baada ya kauli ya Kidawa zinadhihirisha aliitamka kauli yenyewe kinyume na alivyomaanisha. Baada ya kifo cha Lindo, Kidawa alilia kwa uchungu. Kidawa asingejishughulisha kulia iwapo hakumthamini mwanawe.

Hitimisho

Makala imejikita katika kuchunguza suala la upole linavyoweza kudhihirika katika fasihi andishi kwa kuegemea katika riwaya ya *Pendo la karaha*. Uchanganuzi wa kauli za wahusika zinazodhihirisha upole umefanywa kulingana na mikakati ya upole iliyopendekezwa na Brown & Levinson (keshatajwa). Kutohana na mifano ya kauli zinazodhihirisha upole, imebainika kuwa mikakati yote minne ya upole imedhihirika kikamilifu. Vivyo hivyo, imebainika kuwa MCU ndiyo mikakati iliyopendelewa na wahusika katika kuendeleza mawasiliano kupitia kauli za wahusika zinazodhihirisha msemaji kutambua mahitaji ya msikilizaji, kutafuta makubaliano na kujumuishana katika mambo. Imebainika kuwa wahusika mbalimbali walidhihirisha mikakati hii ya upole kupitia kauli walizozitamka kwa lengo la kuimarisha na kudumisha mazungumzo yao. Tofauti za mamlaka, umri, uhusiano na urafiki zinawachangia wahusika kuteua mikakati

mwafaka ya upole. Vile vile, hali ya maisha inayowakabili wahusika kama vile umasikini inachangia mhusika kuteua mkakati wa upole anaouona bora. Kadhalika, imebainika kuwa kuna baadhi ya wahusika wanashindwa kudhihirisha kauli fulani zinapoelekezwa kwao. Majibu yao yanapoenda kinyume na matarajio ya mse maji, utoupole unazuka.

Kutokana na mjadala huu ni bayana ya kwamba suala la upole lina umuhimu mkubwa katika mawanda ya mawasiliano. Suala la upole katika mawasiliano siyo suala tu la kiakademia bali pia la kujenga uhusiano mzuri kati ya washiriki katika mazungumzo. Suala hili linavuka ulimwengu wa kiakademia kwa kuwa ufanisi wa mawasiliano ni jambo lenye uzito katika mustakabali wowote ule wa kimaisha. Katika mawanda ya diplomasia, maswala ya amani, maridhiano katika jamii na hata katika ulingo wa kimataifa, suala la upole linaweza kuwa na uzito mkubwa. Uzito huu unaweza kufanikisha malengo ya wadau katika sekta hizi wanapopania kuboresha shughuli zao.

Marejeleo

- Brown, P. & Levinson, S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage*. Cambridge University Press.
- Goffman, E. (1967). *Interaction Ritual; Essays on Face-to-face behavior*. Doubleday.
- Grice, H. P. (1975). *Logic and Conversation*, In Cole, P. & Morgan, J. *Syntax and Semantics*, vol. 3, Academic Press.
- Gromov, M. D. (2018). Three Novels of John Habwe: Social Criticism through “New Enlightenment”? *Journal of Language, Technology and Entrepreneurship in Africa*, 9(1): 90-100.
- Habwe, J. (2014). *Pendo la Karaha*. Moran East African Publishers Limited.
- Lakoff, R. (1973). *The Logic of Politeness; On minding your p's and q's*. Paper from the 9th Regional Meeting. Chicago Linguistic Society. Chicago Linguistic Society University.
- Leech, J. (1983). *Principles of Pragmatics*. Addison-Wesley.

- Machira, S. (2015). *Uchambuzi wa Mikakati ya Upole kama Inavyotumiwa na Wahusika Wakuu katika Tamthilia ya Mbaya Wetu*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Ngisirei, M. (2018). *Uchambuzi wa Upole katika Vipindi vya Sobetab Kapchi katika idhaa ya Kass FM*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Raitania, A. (2014). *Mikakati ya Upole katika Vipindi vya Runinga: Mawaidha na Bi. Msafwari katika Runinga ya Citizen*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. KAUTTU Limited.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide~Muwa Publishers Limited.
- Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford University Press.